**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'

*Jotham Muyumba [1*]& Dkt. David Kihara, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta S. L. P. 43844 – 00100 Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-3542-0331; Barua pepe ya mawasiliano: muyumbajotham@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*05 Octoba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*KS, Lugha Changizi, Lugha Pokezi, Mashartizuizi, Umbotokeo, Umboghafi, Sheng', S.E.D*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulidhamiria kutathmini athari za kamusi ya *Sheng'* – English Dictionary kwa Kiswahili sanifu. Kamusi ya *Sheng'* – English Dictionary (2003) iliteuliwa kama msingi wa uchunguzi huu kwa sababu ndio kamusi ya kwanza ya *Sheng'* kuwahi kuchapishwa. Licha ya kamusi hii kuchapishwa katika lugha ya Kiingereza ina leksimu za *Sheng'* ambazo yafaa kuchunguzwa namna zinavyoathiri Kiswahili sanifu. Lengo la utafiti huu lilikuwa kueleza muundo wa kifonolojia wa maneno ya *Sheng'* na jinsi yanavyotofautiana na Kiswahili sanifu. Nadharia ya utafiti ilikuwa Nadharia ya Fonolojia Boreshi ambayo inapatikana katika mtazamo mpana wa Nadharia Boreshi iliyoasisiwa na Alan Prince na Paul Smolensky (2003). Hii ni nadharia inayochunguza hatua za ukuaji wa msamiati kutoka hali ghafi hadi ukubalifu wake kupitia kwa vizuizi tofauti. Mahali pa utafiti palikuwa maktabani na mtandaoni. Mbinu ya uchunguzi ikawa kupitia kusikiliza na kusoma makala mbalimbali kuhusu mada hii. Data ilikusanywa kupitia kwa kuchunguza maneno na vidahizo vya maneno kutoka kamusi ya *Sheng'* – English Dictionary (2003). Iliaminika kuwa kamusi hii ingetupa sampuli ya maneno mahsusi ya *Sheng'* ambayo muundo wake huathiri matumizi katika Kiswahili sanifu kwenye jamii ya kisasa. Uchanganuzi wa maelezo ulitegemea mtazamo wa Fonolojia Boreshi katika nadharia ya fonolojia inayoangazia sarufi zalishi. Katika mtazamo huu, uambishaji wa maneno uliangaziwa na jinsi uundaji huo hutawaliwa na vizuizi mbalimbali na sheria za fonolojia. Uwasilishaji wa data ulikuwa kupitia kwa maelezo ya kina, michoro na jedwali. Uchunguzi huu ulidhamiria kuchangia usomi wa Kiswahili kwa kuweka wazi athari za *Sheng'* katika ukuaji wa lugha ya Kiswahili kimsamiati. Kadhalika, utafiti huu utawasaidia wanafunzi kuweka mipaka bayana kati ya msimbo wa *Sheng'* na lugha ya Kiswahili sanifu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

**APA CITATION**

Muyumba, J., & Kihara, D. (2022). Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 373-387. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872.

**CHICAGO CITATION**

Muyumba, Jotham and David Kihara. 2022. "Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 373-387. https://doi.org/10.37284/ jammk.5.1.872.

**HARVARD CITATION**

Muyumba, J., & Kihara, D. (2022) "Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 373-387. doi: 10.37284/jammk.5.1.872.

**IEEE CITATION**

J. Muyumba, & D. Kihara, "Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 373-387, Oct. 2022.

**MLA CITATION**

Muyumba, Jotham & David Kihara. "Muundo wa Kifonolojia wa Maneno ya Sheng'". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Oct. 2022, pp. 373-387, doi:10.37284/jammk.5.1.872.

## UTANGULIZI

Katika makala haya tunadhamiria kueleza miundo ya kifonolojia ya leksimu za *Sheng'*. Tulichunguza vipashio tofauti vya msimbo wa *Sheng'* na jinsi vinavyodhihirika kifonolojia. Miundo ya kifonolojia ya konsonanti za *Sheng'* pamoja na irabu imejadiliwa kwa kina. Istoshe, Sifa bainifu zinazotofautisha irabu na konsonanti za *Sheng'* zimeelezwa. Aidha, miundo ya sauti katika silabi za *Sheng'* imechunguzwa. Tumetumia maneno kutoka S.E.D kueleza miundo hii. Mifano mahsusi imeshughulikiwa hasa kutoka kwa maneno ya S.E.D. Mwisho, sifa za arudhi za *Sheng'* zimejadiliwa. Sifa hizi ni shadda pamoja na toni.

## FONOLOJIA YA *SHENG'*

Mgullu (1999) anaeleza fonolojia kama taaluma maalumu ya isimu ambayo kazi yake ni kuchambua mfumo wa sauti zinazotumika katika lugha fulani. Kwa mujibu wa utafiti huu, msimbo unaorejelewa katika muktadha huu ni msimbo wa *Sheng'*. Mgullu (1999) aliigawa fonolojia katika matawi makuu mawili: Fonolojia vipande sauti na fonolojia arudhi. Fonolojia vipande sauti hujishughulisha katika ubainishaji wa vipandesauti maalum katika lugha fulani. Vipande sauti hivi ni fonimu na alofoni. Kwa mujibu wa utafiti huu, tulijikita katika kuchunguza namna fonimu ya *Sheng'* inavyodhihirika na kuathiri KS. Kwa upande mwingine, Mgullu (1999) alieleza fonolojia arudhi kama taaluma inayoshughulika katika kuchunguza vipashio vikubwa sana vya lugha kuliko fonimu. Vipashio hivi ni mkazo, toni, kiimbo na silabi. Utafiti huu, uliangazia zaidi namna toni na miundo ya silabi inavyojitokeza katika *Sheng'*. Hii ni kwa sababu vipande sauti hivi vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika uundaji wa maneno na maana za maneno katika *Sheng'*.

Kwa hivyo, ilikuwa vyema kuchunguza vigezo hivi vitatu vya fonolojia na namna vinavyojitokeza katika *Sheng'*.

### Fonimu za *Sheng'*

Makini (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alifafanua fonimu kama kitengo cha sauti yoyote ya lugha inayobainishwa kimatamshi katika maneno ya lugha lengwa**.** Mgullu (1999) alitoa ufafanuzi wa sifa bainifu za fonimu. Baadhi ya sifa hizo ni kuwa kila fonimu hushiriki katika kujenga na kutofautisha maana katika neno. Kigezo hiki kilitufaa sana katika uchunguzi wetu kwa sababu tuliweza kubaini namna fonimu mbalimbali zinavyoshiriki kujenga na kutofautisha maana katika msimbo wa *Sheng'*. Tulichunguza namna sauti mbalimbali za vokali na konsonanti zinavyoshiriki katika kujenga na kutofautisha maana katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*.

Kwa mfano, neno la KS *mzee* linabadilika na kuwa *msee* katika *Sheng'*. Kikwamizo ghuna cha ufizi **/z/** kinabadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na kikwamizo cha ufizi sighuna **/s/**. Mabadiliko haya yanatathminiwa na kihimili cha uzalishi cha nadharia ya Fonolojia Boreshi. Sauti /**s**/ na **/z/** zinakuwa maumbo shindani. Sauti hizi zikiingizwa katika *Sheng'* konsonanti **/s/** inakuwa umbotokeo na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

kushiriki katika uundaji wa neno *msee*. Mgullu (1999) alizidi kueleza kuwa, ukibadili fonimu katika neno, maana ya neno hilo itabadilika au kupotea. Aidha, mpangilio wa fonimu kwa baadhi ya maneno ukivurugwa maana ya neno husika itabadilika au kupotea. Dai hili liliafiki uchunguzi wetu kwa sababu, tuliweza kubainisha namna fonimu fulani katika baadhi ya maneno katika data ya utafiti huu inavyobadilika. Katika S.E.D tuligundua maneno kama *gwara* (iba) na *gwaya* (ogopa). Maneno haya yanakaribiana lakini fonimu **/r/** ikibadilishwa na **/y**/, maana kusudiwa huathirika.

Kauli ya mwisho ya Mgullu (1999) kuhusu fonimu kuwa, kila lugha ina fonimu zake na fonimu za lugha mbili tofauti haziwezi kufanana, ilifaa sana katika uchunguzi huu. Kama itakavyodhihirika katika maelezo yafuatayo, tuliweza kuchunguza namna fonimu mbalimbali zinavyoshiriki kuzua tofauti kati ya *Sheng'* na KS. Tuligundua kuwa fonimu za irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** hazipatikani katika KS lakini ziko katika *Sheng'*. Kulingana na Mgullu (1999), kuna taratibu mbalimbali zinazotumiwa kutambua fonimu. Taratibu hizi ni zifuatazo: kufanana kifonetiki, jozi mlinganua finyu, mgawanyo wa kiutoano, na mpishano huru. Kigezo cha fonimu kufanana kifonetiki kilitumika katika utafiti huu kuainisha sauti za irabu na konsonanti za *Sheng'*. Kutokana na data ya utafiti wetu, maneno kama *banɔ* na *bakɔ* yaliainishwa kwa msingi wa kuwa na sauti ya irabu **/ɔ/.**

Irabu hii katika maneno yote mawili inafanana kifonetiki na ilisaidia katika uchunguzi huu kueleza namna fonimu za *Sheng'* zilivyo tofauti na KS. Tulitumia kigezo cha jozi mlinganuo finyu kueleza tofauti ndogo sana zinazojitokeza katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Mgullu (1999) alieleza jozi mlinganua finyu kuwa, ni tofauti ndogo sana ya kifonolojia iliyopo baina ya maneno fulani. Tuliweza kugundua namna irabu **/ɔ/** na **/o/** zinavyochangia kuleta maana tofauti katika neno *bakɔ* (mchezo wa vikapu) na *bak**o*** la KS linalomaanisha (kipimo cha kitanga cha mkono). Utaratibu wa mpishano huru ulitumika katika utafiti huu kubainisha baadhi ya maneno katika *Sheng'* ambayo yana fonimu moja ambayo ni tofauti lakini tofauti hizo hazisababishi tofauti katika maana. Maneno *ma**d**a* na *ma**nd**a* katika S.E.D yote yana maana sawa ya *kuua*. Tofauti inajitokeza katika sauti za silabi **/d/** na **/nd/.**

***Fonimu /ɛ/ katika Sheng'***

Tuligundua kuwa baadhi ya maneno katika *Sheng'* huwa na silabi yenye irabu **/ɛ/.** Baadhi ya maneno tumeyaorodhesha katika *Jedwali 1* lifuatalo.

**Jedwali 1: Fonimu /ɛ/ katika *Sheng'***

| **Maneno katika S.E.D.** | **Maana** |
|---|---|
| Babɛ | Msichana mdogo |
| Gafɛ | Kahawa |
| Palɛ | Rafiki mkuu |
| Kalɛ | Jamii ya Wakalenjin |
| Telɛ | Runinga |

Irabu /ɛ/ haijitokezi katika KS (Mugambi, 2007). Ikitumika katika *Sheng'* hubadilisha matamshi ya maneno kwa kubadili kidatu kinachozua toni katika *Sheng'*. Kuzuka kwa maneno mengi katika *Sheng'* yenye irabu **/ɛ/** huenda kukazua athari za kifonolojia kwa KS. Maneno ya KS yasiyokuwa na toni huenda yakaanza kutamkika yakiwa na toni. Neno kama *kale* (zamani) la KS laweza kutamkika visivyo na kuwa *kalɛ* (jamii ya Kalenjin).

***Fonimu /ɔ/ katika Sheng'***

Kwa mujibu wa utafiti huu, tuligundua kuwa irabu **/ɔ/** hutokana na maneno ya mkopo kutoka Kiingereza na lugha za kienyeji nchini Kenya. Kindija (2012) anaibainisha kuwa irabu ya nusu-chini ya nyuma mviringo. Inapotamkwa, ulimi huwa katikati ya irabu ya chini na irabu ya kati. Kadhalika, ulimi huwa sehemu ya nyuma kabisa kinywani huku mgao wa midomo ukiwa katika umbo la mviringo. Tuligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yaliyokopwa kutoka Kiingereza na kufupishwa, silabi za mwisho huwa na irabu hii.

**Jedwali 2: Fonimu /ɔ/ katika *Sheng'***

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

| Neno | Lugha changizi | Maana |
|---|---|---|
| Bakɔ | Kiingereza – *Basketball* | Mpira wa vikapu |
| Panɔ | Kiingereza – *Punishment* | Adhabu |
| Bayɔ | Kiingereza – *Biology* | Somo la viumbe hai |
| Taɔ | Kiingereza – *Town* | Sehemu ya mji |
| Pangɔ | Kiswahili – Nafasi kubwa katika majabali | Mtaa wa Pangani jijini wa Nairobi |

Kutokana na maelezo haya, irabu **/ɔ/** inajitokeza wazi katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Irabu hii haiko katika KS kwa sababu huzalika kwa wingi kutokana na lugha ya Kiingereza baada ya kudondosha silabi tamati katika neno. Mtindo huu wa kufupisha maneno ya mkopo kutoka Kiingereza kwa kudondosha silabi tamati za neno hauko katika KS. Mtaa wa *Pangani* katika KS unabaki tu kuwa *Pangani* lakini katika *Sheng'* neno hili linafupishwa na kuwa *Pangɔ*. Hali hii husababisha maneno kutamkwa kwa kidatu cha juu ambacho huzalisha toni. Kindija (2012) anaeleza kuwa, lugha nyingi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara huwa na toni. Ni lugha chache tu zisizo na toni ikiwemo lugha ya KS. Kidatu kinachojitokeza katika matamshi ya baadhi ya maneno yenye irabu **/ɔ/** huzua toni.

Toni imepenyezwa katika *Sheng'* kutokana na maneno ya mkopo ambayo yatokana na lugha za fonimu **/ɔ/.** Githiora (2018:93) anaeleza kuwa lugha ya Dholuo huwa na mfumo wa kiambishi **/o/** au **/ɔ/.** Kiambishi hiki huwa kinapachikwa mwanzoni au mwishoni mwa nomino za pekee hasa zinazorejelea mahali au watu mahsusi. Githiora (2018) alitoa mifano ya maneno ya Dholuo kama odukɔɔ (duka), *Oriabaa* (mtaa wa Kariobangi mjini Nairobi), na *Ɔkuyɔɔ* (mtu kutoka jamii ya Gikuyu). Mfumo huu wa sauti ndio uliokopwa na kuingizwa katika msimbo wa *Sheng'*. Nomino za kipekee zinazorejelea mahali katika *Sheng'* zimechukua mkondo huu. Katika data ya utafiti huu maneno kama, *Dagɔ* (mtaa wa Dagorreti) na *Pangɔ* (mtaa wa Pangani) ni baadhi ya mifano. Huenda matumizi makubwa ya irabu **/ɔ/** miongoni mwa vijana yaweza kuhamishwa hadi katika KS. Hali hii ikiendelea basi maneno yenye irabu **/ɔ/** yaweza kuhamishwa kwa kupata matumizi katika KS. Hali hii itachangia katika kufifia kwa KS.

Vokali **z**a ***Sheng'*** Katika Leksimu **z**a **S.E.D**

Mwihaki (2007) alibaini kuwa *Sheng'* inazo vokali saba ambazo ni; ***/a/, /e/, /i/,*** /ɛ /, /ɔ/ na ***/u/*** kama zilivyo katika lugha nyingi za Kibantu. Kiswahili kwa kawaida huwa na vokali tano ambazo ni /a/, /e/, /i/, /o/, na /u/. Hata hivyo, *Sheng'* imekopa vokali */ɛ/ na /ɔ/* kutoka kwa lugha za Kibantu. Vokali inaweza kutumika katika mazingira yoyote ya neno, na inaweza kuambatana na konsonanti yoyote. Vokali hizi zimefafanuliwa zaidi kwa kuzingatia sehemu ya kuzitamkia na mwinuko wa ulimi katika kinywa. Kuhusu mahali pa kutamkia vokali, sehemu tatu hutumiwa kuzitofautisha kama zilivyoainishwa katika Jedwali 3.

**Jedwali 3: Vokali za *Sheng'* (Mugambi, 2007)**

| Mwinuko wa ulimi | Sehemu ya ulimi Mbele | Kati | Nyuma |
|---|---|---|---|
| juu | i | | u |
| kati-juu | e | | o |
| kati- chini | ɛ | | ɔ |
| chini | | a | |

Tulitathmini aina hizi za vokali na kuweza kuzibainisha kutoka baadhi ya maneno yaliyo katika data ya utafiti huu. Kutokana na data katika jedwali hili, irabu /i/, /e/, na /ɛ/ ni za mbele. Irabu /a/ ni ya kati na irabu /u/, /o/ na /ɔ/ ni za nyuma.

Katika utafiti huu, tuligundua baadhi ya maneno ya *Sheng'* ambayo huchukua sauti ya irabu ***/i/*** au ***/e/*** katika tamati mwa maneno. Maneno mengi ni yale yaliyokopwa kutoka Kiingereza, kama inavyoonyeshwa katika *Jedwali 4*:

***Vokali /i/ na /e/ katika Sheng'***

**Jedwali 4: Maneno mkopo ya *Sheng'* katika S.E.D**

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

| **Kiingereza** | ***Sheng'*** | **Maana** |
|---|---|---|
| Dot | Doti | Kuongea visivyo |
| Gang | Gange | Kazi ya kuajiriwa |
| Jersy | Jezi | Shati wanaovaa wachezaji. |
| Maize | Mei | Mahindi |
| Brandy | Brandi | Mpya |

Maneno ya Kiingereza yanayoishia kwa konsonanti hupachikwa irabu ili kuafiki muundo wa silabi wa *Sheng'*. Kwa mujibu wa Mwihaki (2007), silabi nyingi za *Sheng'* huchukua muundo wa KV. Neno *dot* (alama) linapachikwa irabu /**i**/ na kuwa *dot**i*** (kuongea visivyo). Aidha, *gang* (kikosi cha majambazi) nalo linapachikwa irabu /**e**/ na kuwa *gang**e***. Hata hivyo, kuna baadhi ya konsonanti ambazo hulazimika kudondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu. Katika neno *brand**y***, konsonanti */y/* inatolewa na mahali pake kuchukuliwa na irabu ***/i/.*** Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, muundo wa silabi wa KV unachukuliwa kama kihimili cha shartizuizi. Muundo huu unaamua namna silabi zinazotokona na maneno ya mkopo zinavyofaa kujitokeza katika *Sheng'*. Silabi ***ndy*** katika neno *bra**ndy*** linakiuka shartizuizi hili. Inalazimika konsonanti /**y**/ idondoshwe na mahali pake pachukuliwe na irabu /**i**/. Kwa hivyo silabi inayozalika inakuwa **ndi**. Neno mpya linaloundwa na kuwa umbotokeo linakuwa *bra**ndi***. Kwa mujibu wa data ya jedwali la 5 kuhusu maneno ya mkopo, tumeangazia namna irabu /**i**/ na /**e**/ zinavyochangia katika uundaji wa leksimu mpya. Neno asili linalazimika kuchukua irabu hizi katika silabi za tamati mwa neno. Hata hivyo, baadhi ya maneno yanalazimika kuwa na mpangilio wa silabi wa KV. Kutokana na data katika S.E.D, mpangilio huu hujitokeza kwa silabi za mwisho katika baadhi ya maneno. Mfano mzuri unaweza kuonekana kutokana na maneno ya Kiingereza *set* na *plan*.

Maneno haya yanachukua irabu ***/i/*** katika silabi ya mwisho na kuwa *seti* (wekelea) na *plani* (makubaliano) mtawalia. Katika maneno haya, silabi za mwisho zinabadilika kutoka kuwa konsonanti pekee (K) hadi kuwa KV. Konsonanti ***/t/*** katika *se**t*** inatiwa irabu ***/i/*** na kuwa ***-ti.*** Vilevile, konsonanti /**n**/ katika neno *pla**n*** inatiwa irabu ***/i/*** na kuwa ***-ni.*** Mpangilio wa silabi KV linakuwa shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Badala ya silabi za maneno haya kuishia kwa konsonanti, zinaishia kwa irabu kwa kuunda maneno *seti* na *plani* mtawalia. Aidha, neno la Kiingereza *brandy* lenye konsonanti /***y***/ kwa silabi ya mwisho**,** /***y***/ inadondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na irabu /**i**/. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, mhimili wa utathmini unatumika kuamua umbo la silabi itakayoundwa baada ya *Sheng'* kukopa baadhi ya maneno. Maneno ya *Sheng'* yanayoishia kwa konsonanti pekee yanalazimika kupachikwa irabu ili yaafiki muundo wa silabi wa KI.

### *Vokali ndefu katika Sheng'.*

Ferari (2014) alibainisha kuwepo kwa vokali fupi na vokali ndefu katika msimbo wa *Sheng'*. Vokali ndefu hutokea ikiwa irabu moja itajirudia kimfuatano katika silabi. Vokali ndefu ndiye inayobainishwa na Makini (2015) kuwa irabu ya mvuto. Neno la *Sheng' ukoo* (nzuri, muhimu) lina irabu /**o**/ inayotokea mara mbili kwa mfululizo. Vokali hizi huwa huru kama vokali sahili yaani hazifungwi na mazingira ya kifonetiki. Kwa upande mwingine KS huwa tu na vokali fupi. Hata iwapo kuna mfuatano wa irabu katika sehemu ya tamati mwa neno, irabu ya mwisho hutamkika tofauti na kuunda silabi mahsusi. Maneno kama *paa*, *kaa* na *twaa* huchukua umbo hili. Kwa mujibu wa utafiti wetu uvutaji wa silabi hufanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS.

### Konsonanti za *Sheng'*

Mwihaki (2007) na Mugambi (2007) walieleza kuwa konsonanti za *Sheng'* hubainishwa kwa kutumia sifa bainifu kama vile za kimatamshi, kiakustika au kimasikizi. Mgullu (1999) alieleza kuwa, konsonanti huainishwa kwa kuzingatia namna zinavyotamkwa. Katika KS Mgullu (1999) alibainisha konsonanti 24. Naye Mwihaki (2007) akatambua konsonanti 28 katika msimbo wa *Sheng'*. Fonimu za konsonanti za *Sheng'* ni: /b/ /c/ /d/ /f/ /g/ /j/ /k/ /l/ /m/ mb/ /n/ /nd/ /ɲʃ/ /nt/ / ŋ/ /nŋ/ /ð/ /ɲ/ /p/ /r/ /s/ /s/ /t/ /ts/ /θ/ /w/ /v/ /z/. Konsonanti hizi zaweza kuinishwa katika *Jedwali 5* lifuatalo.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

**Jedwali 5: Konsonanti za *Sheng'* (Mwihaki 2007)**

| Jinsi ya kutamka | | Mahali pa kutamkia | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Midomoni** | **Menoni** | **Ufizi** | **Burutioni** | **Kaakaa laini** | **kooni** |
| Vipasuo | Ghuna | b, mb | | d | | g | |
| | Sighuna | p | | t/ nt | | k, c | |
| Vizuiwa | Ghuna | | | | J | | |
| | Sighuna | | | | Ð | | |
| Vikwaruzo | Ghuna | v | ð | z | | | |
| | Sighuna | f | θ | S, ts | Š | | |
| Nazali | Ghuna | | m | | N | ɲ | ɳ |
| | Sighuna | | | | | | |
| Vilainisho | Ghuna | | | l, r | | | |
| Viyeyusho | Ghuna | | | | | | |
| | Sighuna | | | | | y | w |

Tulipolinganisha konsonanti za *Sheng'* na za KS kwa mujibu wa Mgullu (1999) na kisha Mwihaki (2007), tulibaini kuwa kuna konsonanti za *Sheng'* ambazo hazipatikani katika KS nazo ni*: nt, ts, ɲʃ,* na *c*. Tuligundua maneno yafuatayo kutoka S.E.D ambayo yameundwa kwa sauti za konsonanti hizi.

**Jedwali 6: Konsonanti za *Sheng'* katika S.E.D ambazo hazipatikani katika KS**

| Neno | Konsonanti | Maana |
|---|---|---|
| Njeve | ɲʃ | Baridi |
| Inosenje | ɲʃ | Kuwa bila hatia |
| Janta | nt | Kazi ambayo mtu ameajiriwa kufanya |
| Anti | nt | Mwanamke wa heshima |
| Chintu | nt | Msichana mdogo |

Licha ya kuwa (Mugambi 2007) alibainisha sauti ***nt***, ***ts***, ***ɲʃ***, na ***c*** hatujapata maneno yanayoundwa na konsonanti hizi. Sababu kuu huenda ikawa wachapishaji wa KS huhofia kukiuka muundo wa silabi za KS. Hata hivyo, licha ya maneno haya kuwa katika S.E.D, hayajajitokeza katika machapisho ya KS. Uchanganuzi wa fonimu za *Sheng'* umetudhihirishia kuwa vokali na konsonanti kwa ujumla huchukua maumbo na miundo tofauti. Uhusiano wa vokali na konsonanti utazidi kujitokeza katika uchanganuzi ufuatao wa ruwaza za sauti katika silabi. Sauti hizi zitachangia katika utafiti huu kwa sababu zitatumika kuonyesha namna fonolojia ya *Sheng'* ilivyo tofauti na KS. Tofauti hizi kadhalika, zaonyesha uwezekano wa fonimu za *Sheng'* kuathiri KS.

**Silabi za *Sheng'***

Baada ya kuchanganua fonimu za *Sheng'* tuliona kuwa, ni vyema kutathmini namna fonimu hizi huunda silabi za *Sheng'*. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), fonimu zinapokaa pamoja hujenga silabi ambazo huweza kutamkwa kama kitu kimoja. Kila lugha huwa na muundo wake wa silabi. Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya ya Mgullu (1999), msimbo wa *Sheng'* vilevile una miundo yake mbalimbali ya silabi.

Kwanza, tulirejelea maelezo ya Mgullu (1999) na tukagawa silabi za *Sheng'* katika makundi mawili; silabi funge na silabi wazi. Silabi funge kwa mujibu wa Mgullu (1999), ni zile ambazo huishia kwa konsonanti. Matamshi ya silabi funge hukatika ghafla. Silabi wazi ni zile ambazo huishia kwa irabu. Zinapotamkwa matamshi hayakatiki kwa haraka au ghafla. Makini (2015) katika tasnifu yake ya uzamili, alieleza kuwa silabi wazi ni zile ambazo hazina kifungio. Silabi za aina hii kwa kawaida huwa na vokali mwishoni ambayo hujenga kilele cha silabi hiyo. Baada ya kugawa silabi katika aina mbili kuu, Mgullu (1999), aliweza kubainisha aina saba kuu za miundo ya silabi za KS. Nazo ni: konsonanti irabu (KI), irabu pekee (I), konsonanti

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

pekee (K), konsonanti konsonanti irabu (KKI), konsonanti, nusu irabu, irabu ($K\frac{1}{2}II$), konsonanti konsonanti, nusu irabu, konsonanti ($KK\frac{1}{2}IK$), na mwishowe silabi funge. Uainishaji huu wa Mgullu (1999), ulifaa sana katika utafiti huu kwa sababu ulitumika kulinganisha miundo ya silabi za KS na miundo ya silabi za *Sheng'* ilivyobainishwa na Mwihaki (2007).

Aidha, miundo hii ya silabi za KS imechukuliwa kama mashartizuizi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kila neno la KS lazima lichukue muundo huu wa silabi. Maneno ambayo yanakiuka utaratibu wa muundo huu yanatupiliwa mbali. Kwa hivyo, hayawezi kukubalika katika KS kama umbotokeo. Maneno mengi ya *Sheng'* huundwa kwa silabi wazi. Tuliweza kubainisha aina hizi za silabi katika data ya utafiti huu.

**Jedwali 7: Silabi funge na silabi wazi katika S.E.D**

| Maneno katika S.E.D. | Lugha changizi | Magao wa silabi | Aina ya silabi |
|---|---|---|---|
| Kinda | Kiswahili | Ki-nda | Silabi wazi, silabi wazi |
| Kuli | Kiswahili | Ku-li | Silabi wazi, silabi wazi |
| Plani | Kiingereza | Pla-ni | Silabi wazi, silabi wazi |
| Stadi | Kiingereza | Sta-di | Silabi wazi, silabi wazi |
| Stori | Kiingereza | Sto-ri | Silabi wazi, silabi wazi |
| Maskani | Kiswahili | Mas-ka-ni | Silabi funge, silabi wazi, silabi wazi |

Kutokana na maneno yaliyo katika jedwali hili, tuligundua kuwa maneno mengi ya *Sheng'* huundwa kwa silabi wazi. Hata maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiingereza, na yanaoishia kwa silabi ya konsonanti tu, hulazimika kuchukua irabu na kuwa silabi wazi. Huenda sababu kuu ni kufanya matamshi ya silabi hizi yaafikiane na muundo wa KI unaojitokeza kwa wingi katika silabi za KS na lugha za Kibantu. Tulitumia uainishaji wa Mwihaki (2007) kubainisha aina tofauti za silabi za *Sheng'*. Silabi hizi ni: KI, KIK, I, N, IK na KKI. Mifano imetolewa katika *Jedwali 8* lifuatalo.

**Jedwali 8: Miundo ya silabi za *Sheng'***

| Muundo wa silabi za *Sheng'* | Neno katika S.E.D. | Maana |
|---|---|---|
| KI, | **Ja-**ka | Mtu kutoka jamii ya Wajaluo |
| KIK | **Ma-s**kani | Chumba cha kujificha |
| I | **O-**na | Piga kofi |
| N | **M-**zizi | Mmea wa kulevya |
| IK | **Ar-**me | Wanajeshi |
| KKI | **Bra-**ndi | Mpya |

Githiora (2018) anaunga mkono dai hili kwa kuonyesha kuwa sauti */**sh**/* na */**ch**/* hujitokeza kwa wingi sana kama kiambishi tamati kwa maneno mengi ya *Sheng'*. Maneno kama *odu**sh*** kwa maana ya *jiwe* na *Kibi**ch*** kwa maana ya *Kibera* huchukua umbo hili. Inaaminika kuwa matamshi ya irabu huwa hayakatiki kwa haraka kama yale ya konsonanti na kwa hali kama hiyo silabi wazi huonekana kama ipo huru au wazi zaidi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa data ya utafiti huu tuligundua kuwa maneno ya S.E.D yanayopatikana katika KS hulazimika kuchukua irabu kwa silabi zinazoisha kwa konsonanti. Hali hii hufanya silabi nyingi za *Sheng'* kuwa wazi ilhali umbo asili ni silabi funge. Kama tulivyofafanua pale juu, neno kama *seti* latokana na *set* la Kiinegereza. Konsonanti ***/t/*** inaambatanishwa irabu ***/i/*** na kubadili na kuunda silabi wazi. Aidha, maneno ya Kiingereza *plan* na *dot* yanachukua umbo la silabi wazi na kuwa *plan**i*** na *dot**i*** mtawalia. Hata hivyo, tulipochunguza S.E.D kwa makini tulibainisha maneno mengi ya *Sheng'* ambayo yana silabi funge. Jedwali lifuatalo linadhihirisha mifano ya maneno hayo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

**Jedwali 9: Silabi funge za *Sheng'* katika S.E.D.**

| Neno | Silabi funge | Maana |
|---|---|---|
| Baksi | -bak- (KIK) | Kutulia/kupumzika |
| Beksi | -bek- (KIK) | Shilingi moja |
| Bangla | -bang- (KIK) | Mtaa wa Kariobangi |
| Boksa | -bok- (KIK) | Chupi ya wanaume |
| Fasta | -fas- (KIK) | Harakisha |

***Silabi za Vitenzi vya Sheng'***

Vitenzi vingi vya *Sheng'* hukopwa kutoka kwa lugha zingine. Baadhi hutokana na vitenzi vya KS, lugha za Kibantu na Kiingereza. Kama ilivyo katika KS tuligundua kuwa, baadhi ya vitenzi huchukua silabi ***ku*** kama kiambishi awali kabla ya mzizi. Tulibainisha mifano kutoka S.E.D kama inavyoonyeshwa katika *Jedwali 10*.

**Jedwali 10: Vitenzi katika *Sheng'***

| Kitenzi | Kiambishi ku | Maana |
|---|---|---|
| Manga | Kumanga | Kula chakula |
| Dinda | Kudinda | Kataa kwa kiburi |
| Sanya | Kusanya | Iba |
| Mada | Kumada | Ua |
| Choma | Kujichoma | Kuanzisha mradi halafu ushindwe kukamilika |
| Seti | Kujiseti | Kuwa tayari |

Jedwali hili la vitenzi katika *Sheng'* linaonyesha namna vitenzi huchukua kiambishi ***ku*** katika kauli ya kutenda kama kiambishi awali. Muundo huu wa silabi unakaribiana sana na KS. Hata hivyo, katika S.E.D tuligundua kuwa baadhi ya vitenzi vilivyokopwa kutoka Kiingereza huhifadhi umbo lake asili kabla ya kuchukua silabi ***ku***. Kitenzi *seti* (kuwa tayari) kinatokana na kitenzi cha Kiingereza *set* chenye maana pia ya *kuandaa mpangilio*. Kinavyoingizwa katika *Sheng'* umbo la silabi linabadilishwa ili kuafiki mpangilio wa silabi za *Sheng'* za KI. Kwa hivyo badala ya kuandika *kujise**t*** kitenzi kinabadilishwa na kuwa *kujise**ti***. Mpangilio huu wa silabi za *Sheng'* unatimiza mhimili wa shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Hii ni kwa sababu kuwepo kwa irabu katika silabi ni sharti ambalo yafaa litimizwe. Muundo wa silabi za *Sheng'* wa KI unakuwa kigezo cha kuamua ni umbo gani la silabi linakubaliwa. Katika muktadha huu, kitenzi *kujise**t*** linakuwa na silabi ya konsonanti pekee katika tamati mwa kitenzi. Inabidi irabu ***/i/*** iongezwe kwa konsonanti ***/t/*** na kuunda silabi ya muundo wa **KI** ambayo ni ***/ti/***. Kitenzi *kujise**ti*** kinakuwa umbotokeo kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Vitenzi vya KS kama ***ku**la*, ***ku**nywa* au ***ku**cheza* huchukua utaratibu huu.

Hata hivyo silabi ***ku*** hupachikwa kwa vitenzi vya mkopo bila kubadilisha sauti za silabi ili kuafiki mfumo wa KS. Kitenzi cha Kiingereza kama vile *dead* (kufa) kinakuwa ***ku**dedi* (kukufa). Kuna baadhi ya mifumo mingine ya vitenzi hasa vilivyokopwa kutoka Kiingereza ambavyo havijachapishwa katika S.E.D. Vitenzi vilivyohifadhi maumbo asilia ya Kiingereza na kuchukua silabi za *Sheng'* kama viambishi, havikuchapishwa. Vitenzi kama; ***ku**relax*, ***ku**jienjoy*, ***ku**fight* na ***ku**travel* havijachapishwa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Fonolojia Boreshi, kuna shartizuizi kuwa muundo wa silabi za *Sheng'* lazima uchukue mkondo wa KV. Vitenzi visivyochukua umbo hili vinapuuziliwa mbali.

Ferrari (2014) aligundua kiambishi cha hali isiyodhihirika ***nga*** katika *Sheng'*. Kiambishi hiki hujitokeza katika baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vya zamani. Kitenzi kama hufinya***nga*** huchukua mkondo huu. Hata hivyo katika *Sheng'* kiambishi ***nga*** kinatumika katika hali zote za nyakati na hali. Ikiwa kitenzi katika hali ya kutenda huishia kwa irabu ***/a/*** basi silabi ***nga*** hupachikwa kwenye kitenzi. Hata hivyo, ikiwa kitenzi kina irabu ***/i/*** basi silabi ***ngi*** itatumika. Kigezo hiki kinafanya silabi hii

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

kuzua tofauti kubwa kati ya KS na *Sheng'*. Katika ukanushi, kiambishi hiki hubadilika na kuwa ***ngi***. Tulipochunguza baadhi ya vitenzi katika S.E.D, tuligundua kuwa kuna vitenzi fulani ambavyo vyaweza kuchukua silabi ***nga*** katika kuonyesha nyakati na hali tofauti katika sentensi. Tulijaribu kunyambua vitenzi vinavyopatikana katika data ya utafiti huu ili kutathmini ikiwa maelezo ya Ferrari (2014) yanaafikiwa. *Jedwali 11* lifuatalo linatoa taswira halisi ya uchunguzi wetu.

**Jedwali 11: Silabi nga ya ukanushi katika S.E.D.**

| Kitenzi katika S.E. D | Sentensi katika KS | Sentensi katika *Sheng'* | Ukanushi katika *Sheng'* |
|---|---|---|---|
| Mezea. | Anamezea chakula. | Anamezeanga ukweli. | Hamezeangi ukweli. |
| Penya. | Alipenya katika umati | Amepenyanga na kupotea. | Hapenyangi na kupotea |
| Shiriki. | Hushiriki kanisani mwetu. | Anashirikingi akipewa pombe. | Hashirikingi akipewa pombe |
| Seti. | Alipanga viti katika | Amejisetingi kuanza kampeni. | Hajisetingi kuanza kampeni orodha ya seti tatu. |

Katika jedwali hili, tumeonyesha namna viambishi vya hali na nyakati vinavyobadilishwa katika vitenzi vya KS na mahali pake kuchukuliwa na kiambishi ***nga*** na ***ngi*** katika *Sheng'*.

Katika hali ya ukanushi, kiambishi ***ngi*** hutumika kama kiambishi tamati katika vitenzi vya *Sheng'*. Kiambishi ***nga*** na ***ngi*** hutumika kama mashartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Viambishi hivi vinaamua ni aina gani ya maneno yanayoweza kuzalika katika *Sheng'* yenye silabi tamati ***nga*** na ***ngi***. Maneno yanayoundwa katika *Sheng'* yenye viambishi hivi basi huwa umbotokeo. Hali hii ni tofauti na KS kwa sababu katika KS, vitenzi vya hali ya ukanushi huchukua kiambishi tamati ***-ki***.

### *Silabi za Vivumishi vya Sheng'*

Vivumishi vingi baada ya kukopwa hubadilishwa kwa kuchukua viambishi tofauti ili kuleta upatanisho wa kisarufi katika *Sheng'*. Tulijaribu kuchunguza baadhi ya miundo ya silabi za vivumishi katika S.E.D. Matokeo ni kama yafuatavyo.

**Jedwali 12: Vivumishi katika S.E.D**

| Maneno katika KS. | Kivumishi katika *Sheng'* | Lugha asilia |
|---|---|---|
| Supuu | M-supuu –mrembo sana | Kiingereza - super |
| Poa | M-poa- mzuri | Kiswahili – poa |
| Chafu | M-chafu – mtaalamu | Kiswahili - mwovu/mwerevu |
| Fala | M-fala – asiyejua kusoma | Kiswahili -Mpumbavu na kuandika |
| Zubaa | M-zubao- changanyikiwa | Kiswahili -hali ya bumbuazi akili |

Kutokana na data hii, kipasuo ghuna cha mdomo ***/m/*** kikitiwa kwa baadhi ya nomino na vitenzi kabla ya mzizi, hubadilisha maneno hayo na kuwa vivumishi. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, kipasuo ghuna cha mdomo ***/m/*** kinatumika kama kihimili cha utathmini. Kinashiriki katika kuamua ni aina gani ya vivumishi vinavyoweza kuzalika kutoka kwa nomino za *Sheng'*. Maneno yaliyoorodheshwa katika jedwali la vivumishi katika S.E.D, yanatumika kama umboghafi. Vivumishi vinavyozalika vinakuwa umbotokeo. Hali hii ni tofauti sana na KS ambapo viambishi vya maneno kama ***mwa****-na* hutumika. Neno *jeshi* linakuwa ***mwa****najeshi*. Matumizi mapana ya kipasuo cha midomo **/m/** yakizoeleka pakubwa huenda yakapata matumizi katika KS. Hali hii yaweza kuchangia katika kufifia kwa KS.

### *Silabi za Vielezi katika Sheng'*

Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihirisha kuwa vielezi vingi vya *Sheng'* huundwa kutoka kwa nomino au vivumishi ambavyo hukopwa kutoka

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

lugha zingine. Kiambishi ***ki*** au ***vi*** kinapotiwa kwa baadhi ya nomino na vitenzi, hubadilika na kuwa vielezi.

**Jedwali 13: Muundo wa vielezi katika *Sheng'***

| Maneno asili | Vielezi | Kamusi ya *Sheng'* | Kamusi Sanifu |
|---|---|---|---|
| Orodha -Kiswahili | Kiorodha | Kuwa karibu, | Mpangilio wa majina/vitu zunguka karibu |
| Poa – Kiswahili | Vipoa | Kuwa sawa | Tulia |
| Sure - Kiingereza | Kishua | Kuwa nzuri | Mashua ndogo |
| Radar – Kiingereza | Kirada | Kuwa katika mazingira | Kifaa cha kuongoza meli au ndege |
| Fala – Kiswahili | Kifala | Mjinga | Mpumbavu/bozi |
| Chizi – Kiswahili | Kichizi | Wazimu | Mwenye akili punguani |

Maneno ya S.E.D kama vile *orodha*, *poa*, na *shua* yanaweza kuchukua silabi ***ki*** au ***vi*** na kubadilika kuwa vielezi. Kielezi *poa* kikichukua silabi ***vi*** kinabadilika na kuwa kielezi ***vi****poa*. Mfano huu waweza kudhihirika katika sentensi; *yule odijo hufunza* ***vi****poa* (Yule mwalimu hufunza vizuri). Nomino *fala* inakuwa ***ki****fala* na *chizi* linakuwa ***ki****chizi*. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, viambishi ***ki*** na ***vi*** vinatumika kama mhimili wa utathmini. Vinachangia kuamua ni umbo gani la vielezi vinavyoweza kuundwa baada ya kuchukua viambishi awali ***ki*** na ***vi***. Mkururo huu huenda ndio hufanya wazungumzaji wa *Sheng'* kutumia baadhi ya nomino na vitenzi kama vielezi. Uzoefu mkubwa wa maneno ya sampuli hii yaweza kuathiri leksimu za KS.

***Dhana ya Ukanushi katika Sheng'***

Ferrari (2014) alichunguza namna dhana ya ukanushi inavyojitokeza katika *Sheng'*. Ukanushi wa *Sheng'* hufanana na wa KS. Hata hivyo fonimu za ukanushi ***ha*** na ***hu*** hubadilika na nafasi yake kuchukuliwa na irabu **/a/** au **/i/**. Konsonanti /**h**/ hudondoshwa na sauti za irabu huchukua mahali pake. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, tulibainisha vitenzi vifuatavyo ambavyo huchukua mkururo huu wa ukanushi.

**Jedwali 14: Ukanushi katika *Sheng'***

| Kitenzi katika <u>S.E.D</u>. | Yakinishi | Kukanusha katika *Sheng'* |
|---|---|---|
| Ambaa | Mtoii anaambaa<br>(Mtoto anaondoka) | Mtoii haambai-<br>(Mtoto haondoki) |
| Choma | Mgeni anachoma fegi<br>(mgeni anavuta sigara) | Mgeni hachomi fegi<br>(Mgeni havuti sigara) |
| Dinda | Abiria adinda kusafiri<br>(Abiria akataa kusafiri) | Abiria hadindi kusafiri.<br>(Abiria hajakataa kusafiri) |
| Lenga | Rafiki yake amemlenga<br>(Rafiki wake anajifanya hamuoni) | Rafiki yake hamlengi<br>(Rafiki yake hajifanyi anamuona) |
| Ng'oka | Mgonjwa ameng'oka<br>(Mgonjwa amekufa) | Mgonjwa hajang'oka<br>(Mgonjwa hajakufa) |

Mifano ya sentensi katika jedwali hili la ukanushi katika *Sheng'*, inaonyesha namna sauti ya vokali **/a/** hutumika katika ukanushi katika *Sheng'*. Hii ni mojawapo ya sifa inayofanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS. Mazoea ya aina hii yakishamiri, yaweza kufanya wazungumzaji kupuuza matumizi ya maneno ya KS yenye konsonanti **/h/.** Vokali **/a/** yatumika katika data hii kama kihimili cha utathmini katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Kinatumika kuamua aina za vitenzi vinavyoweza kuzalika katika hali ya ukanushi kikitokea mwanzoni mwa vitenzi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

**MIFANYIKO YA KIFONOLOJIA KATIKA *SHENG'***

Fonimu za *Sheng'* hushiriki katika ujenzi wa maumbo mbalimbali ya viambishi na silabi. Mifanyiko hii huchangia katika kuzuka kwa leksimu mpya za maneno ambayo hupata maana pana katika mawasiliano. Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihirisha mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia.

**Kuhafifika kwa fonimu**

Owino (2016) na Mgullu (1999) wanaeleza kuwa, mfanyiko huu unahusu fonimu kubadilika kutoka kwa fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi na kuwa fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali. Katika utafiti wetu mfanyiko huu ulibainika kutokea kwenye maneno kama vile:

**Jedwali 15: Fonimu za udogo katika maneno ya S.E.D**

| Nomino katika S.E.D. | Udogo katika KS | Udogo katika S.E.D. | Maana |
|---|---|---|---|
| Babe | Kijibabe | Kababe | Msichana mdogo |
| Bano | Kijibano | Kabano | Aina fulani ya jiwe |
| Buyu | Kijibuyu | Kabuyu | Baba |
| Chizi | Kijizi | Kachizi | Wazimu |
| Buda mdogo | Kibuda | Kabuda | Mwanamme mzee |
| Fala | Kijifala | Kafala | Asiyejua kusoma na kuandika |

Kutokana na data katika jedwali la fonimu za udogo, imedhihirika kuwa irabu /**i**/ katika silabi ***ki*** inadondoshwa na mahali pake kuchukuliwa na irabu /**a**/. Katika matamshi, irabu /**a/** hutamkika kwa sauti hafifu ikilinganishwa na /**i**/.

Fonimu ya udogo /**a/** inatumika kama shartizuizi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Ni nomino zinazoweza kuchukua fonimu ***/a/*** ya udogo katika *Sheng'* ndizo hukubalika.

**Usilimishwaji wa Fonimu**

Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulidhihirisha usimilishwaji wa baadhi ya fonimu zinazotamkika katika mazingira jirani. Kipashio jirani huweza kuathiriwa na kipashio kingine kilicho mkabala nacho na hivyo kuchukua sifa za kimatamshi za kipashio hicho jirani. Owino (2016) katika tasnifu yake ya uzamili, alieleza kuwa usilimishwaji unaweza kutokea konsonanti ikiathiri vokali au vokali ikiathiri konsonanti au vokali ikiathiri vokali nyingine au hata konsonanti ikiathiri konsonanti nyingine.

Usilimishwaji ulibainika katika mifano ifuatayo: *wa**z**ee* – *wa**s**ee* (sauti ***/z/*** kubadilika na kuwa /***s/***). Jersy – jazi (sauti ***/s/*** kubadilika na kuwa ***/z/***. Na vile vile ***P**ano* **-** ***b**ano* ambapo sauti ***/p/*** inabadilika na kuwa ***/b/.*** Katika wingi wa nomino hasa katika ngeli ya *A-WA* tuligundua kuwa, KS huwa na kiambishi *wa* cha wingi. Katika *Sheng'* kiambishi hiki hubadilika na kuwa ***ma***. Kiyeyusho **/w/** hubadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na kipasuo cha midomo **/m/.** Muundo wa wingi katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* ulidhihiriswa na maelezo ya Bosire (2006).

Bosire (2006) alitathmini namna nomino zisizokuwa na umbo la wingi na umoja katika KS huwa zinabadilika na kuchukua kiambishi **/m/** katika *Sheng'*. Aidha, nomino za mkopo hasa kutoka lugha ya Kiingereza zikijitokeza katika *Sheng'* huchukua silabi ***ma*** kama kiambishi cha wingi. Alitoa mfano wa neno *ndizi* ambalo katika wingi hubadilika na kuwa ***ma**ndizi*. Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, tuligundua kuwa baadhi ya nomino katika S.E.D zaweza kuchukua muundo huu katika wingi.

**Jedwali 16: Umbo la wingi la nomino katika S.E.D**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

| Nomino katika S.E.D. | Wingi katika *Sheng'* |
|---|---|
| Babe | Mababe |
| Bano | Mabano |
| Buyu | Mabuyu |
| Chizi | Majizi |
| Dafu | Madafu |
| Fala | Mafala |
| Gomba | Magomba |
| Kuli | Makuli |
| Mchuma | Machuma |

Kutokana na jedwali hili ni wazi kuwa, baadhi ya nomino katika *Sheng'* huchukua silabi ***wa*** kama kiambishi awali kwa nomino ili kutoa dhana ya wingi. Hata hivyo, tuligundua kuwa baadhi ya nomino zinakiuka utaratibu huu. Nomino kama *mtumba* haiwezi kuwa ***ma****tumba* bali huwa *mitumba*. Mpishano kati ya neno *mtumba* na *mitumba* inadhihirisha mhimili wa uzalishi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Katika kihimili hiki, maneno haya yanashindana kama umboghafi. Baada ya ushindani huu, neno *mitumba* linakubalika kama umbotokeo baada ya kupitia kwa shartizuizi la kiambishi cha wingi ***mi*** katika *Sheng'*.

**Udondoshaji wa Silabi katika Maneno ya S.E.D.**

Mgullu (1999) alieleza jinsi irabu hudondoshwa katika KS na kuunda sauti tofauti za maneno. Kutokana na data ya utafiti huu, tuligundua maneno mengi katika S.E.D hayadondoshi irabu jinsi Mgullu (1999) alivyoeleza katika KS. Badala ya *Sheng'* kudondosha irabu, tuligundua kuwa, udondoshaji wa silabi nzima ndio hujitokeza kwa wingi kwa baadhi ya maneno. Mifano ifuatayo inaonyesha maelezo haya:

Panga – Pangani (Silabi ***ni*** imedondoshwa)

Kiswa – Kiswahili (silabi ***hi*** na ***li*** zimedondoshwa)

Nai – Nairobi (silabi ***ro*** na ***bi*** zimedondoshwa)

**Tangamano la Irabu katika *Sheng'***

Kulingana na Mgullu (1999), huu ni utaratibu ambao irabu fulani hukubali kuandamana katika mazingira maalum. Katika maneno ya S.E.D kuna baadhi ya irabu ambazo huwa katika mzizi wa neno. Irabu hizi zinajitokeza vilevile kwa baadhi ya viambishi tamati ikiwa neno linanyambuliwa katika hali tofauti. Katika vitenzi vya *Sheng'* vyenye irabu **/o/** kwa mzizi, tuligundua kuwa irabu hii huhusika katika kuunda viambishi tofauti. Neno *ch**o**ma* linakuwa *ch**o**m**o**ka* na *t**o**b**o**a* linakuwa *t**o**b**o**ka*. Kutokana na mifano hii, irabu **/o/** inashiriki kuunda mzizi wa neno na kisha kuunda viambishi.

**SIFA ZA ARUDHI ZA *SHENG'***

Makini (2015) anaeleza sifa arudhi kuwa ni zile zinazowekwa kwenye vipashio vikubwa zaidi ya fonimu. Sifa hizi huwa kwenye silabi, neno, kirai au sentensi. Mifano ya sifa arudhi ni shadda, toni na kiimbo.

**Jinsi Shadda Inavyojitokeza katika *Sheng'*.**

Kindija (2012), alieleza kuwa shadda ni utamkaji wa nguvu zaidi katika sehemu ya neno au fungu la maneno. Makini (2015) anaendelea kusema kuwa, utamkaji wa nguvu hufanywa kwenye silabi kuliko sehemu nyingine yoyote ile. Shadda huweza kuwa na msisitizo au ubainishaji wa maana za maneno. Maneno ya KS hutiwa shadaa katika silabi ya pili kuanzia mwisho mwa neno. Katika neno *m**ko**no*, shadda itatiwa kwa silabi ***ko*** kwa sababu ni ya pili kuanzia mwisho wa neno.

Baadhi ya maneno katika *Sheng'* pia huchukua shadda kwenye silabi ya pili kutoka mwisho. Maneno kama ***chu**ja* (vyatu) na *chi**zi**ka* (kuwa wazimu) hutiwa shadda kwa silabi ya pili kuanzia mwisho. Hata hivyo, tuligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* huwa na shadda mwishoni mwa neno. Githiora (2018) ana mtazamo kuwa wakati ambapo irabu ya mwisho inavutwa, shadda huhamishwa kutoka silabi ya pili kuanzia mwisho. Irabu za tamati ndizo hutiwa shadda kwa sababu huwa na uzito wa sauti kimatamshi. Maneno yenye sauti ya mvuto kama *amba**a*** hutiwa shadda kwa irabu ya mwisho **/a/** inayochukua nafasi ya silabi ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

tamati. Hata hivyo, tulipochunguza S.E.D tulipata mifano zaidi japo haijachapishwa katika KS.

**Jedwali 17: Shadda katika maneno ya *Sheng'***

| Neno katika S.E.D | Silabi iliyotiwa shadda katika *Sheng'* | Silabi iliyotiwa shadda katika KS |
|---|---|---|
| Ambaa | A-mba- 'a | a- 'mba-a |
| Seti | Se- 'ti | 'Se-ti |
| Bako | Ba- 'ko | 'Ba-ko |
| Pango | Pa – 'ngo | 'Pa- ngo |
| Tele | Te- 'le | 'Te- le |

Kutokana na maneno yaliyo katika jedwali hili la shadda, tuligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* hutiwa shadda katika silabi ya mwisho mwa neno. Hali hii ni tofauti mno na jinsi ilivyo katika KS. Mgullu (1999) alieleza kuwa mkazo katika KS hutiwa katika silabi ya pili kuanzia mwisho. Kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi, mhimili wa shartizuizi la KS kuwa silabi ya pili kuanzia mwisho mwa neno ndilo hutiwa shadda unakiukwa neno hilo likikopwa katika *Sheng'*. Shadda ikitiwa tamati mwa neno, hufanya muundo wa kifonolojia wa *Sheng'* kuwa tofauti na ule wa KS. Maneno mengi ya mkopo kutoka Kiingereza yana shadda katika silabi tamati. Kuna hatari kuwa wazungumzaji wa KS wanaweza kuathirika kwa kutia shadda katika silabi tamati kwa hivyo kuathiri mfumo wa matamshi ya maneno katika KS. Tulibainisha maneno yafuatayo katika S.E.D ambayo shadda hutiwa kwa silabi tamati.

**Jedwali 18: Shadda katika silabi tamati katika *Sheng'***

| Neno | Maana |
|---|---|
| Ba'ko | Mpira wa vikapu |
| Ba'ngo | Shilingi moja |
| Ba'no | Aina fulani ya jiwe |
| Mzuba'o | Changanyikiwa akili |
| Pe'po | Adhabu |

**Kiimbo katika *Sheng'*.**

Kindija (2012) akimnukuu Massamba (2004), alieleza kiimbo kama umbo la sauti linalotokana na mpandoshuka wa sauti za maneno wakati wa usemaji. Kiimbo ni utaratibu wa kupanda au kushusha sauti katika usemaji. Kwa mujibu wa Kindija (2012), kiimbo hufanya sehemu fulani za sentensi kusikika zaidi kuliko zingine. Kimsingi, hujumuisha mambo yote yanayohusiana na uzungumzaji, kama kidatu, shadda na toni. Utafiti huu uligundua kuwa, kiimbo katika *Sheng'* huwa na mfanano mkubwa sana na KS. Hata hivyo, namna maneno fulani yanavyotumika katika mawasiliano ya *Sheng'* yanaweza kuzua maana tofauti au kufanya kauli fulani isieleweke ipasavyo.

Tuliweza kugundua kuwa neno kama *sasa* laweza kudhihirisha maana tofauti kutegemea namna kiimbo kilivyotiwa katika mazungumzo. Tuliweza kubainisha aina zifuatazo za viimbo katika *Sheng'* kama inavyoonyeshwa katika jedwali hili.

**Jedwali 19: Kiimbo katika maneno ya S.E.D**

| Aina ya kiimbo | Neno | Sentensi |
|---|---|---|
| Kiimbo kauli | Sasa | Kuja sasa. |
| Kiimbo cha maulizo | Sasa | Utakuja sasa? |
| Kiimbo cha amri | Sasa | Ondokeni sasa. |
| Kiimbo cha mshangao | Jo | Amefika sasa jo! |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

**Toni katika *Sheng'***

Kindija (2012) akimnukuu Massamba (2004) anaeleza toni kuwa, ni kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi ambacho chaweza kubadilisha maana. Kindija (2012) alisisitiza kuwa, toni huambatana na vitamkwa ghuna katika neno na wala sio vitamkwa sighuna. Ili toni ijitokeze katika neno, lazima vitamkwa ghuna viambatane na irabu. Kwa msingi wa maelezo haya, irabu ndizo hubeba toni katika silabi. Kauli hii inaafiki sana utafiti huu kwa sababu tuliweza kubainisha baadhi ya maneno katika S.E.D ambayo yanakuwa na maana tofauti kwa sababu ya toni. Kwa mfano neno *zima* linakuwa na maana mbili. Likitamkwa bila toni linamaanisha *tuliza*.

Hata hivyo toni ikitiwa kwa irabu **/a/** inabadilisha maana ya neno na kuwa *zim**a*** lenye maana ya mtaa wa Zimmerman mjini Nairobi. Kama zilivyo lugha za Kibantu, msimbo wa *Sheng'* huwa na toni. Hali hii inafanya *Sheng'* kuwa tofauti na KS. Kadhalika, katika uchambuzi wa data ya utafiti huu, tuligundua kuwa baadhi ya maneno ya *Sheng'* yaliyokopwa kutoka kwa lugha za Kibantu na Kiingereza huwa na toni. Sauti ya irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** husababisha toni katika baadhi ya maneno ya *Sheng'*. Kutokea kwa irabu **/ɛ/** na **/ɔ/** katika *Sheng'* kunatimiza mhimili wa uzalishi katika nadharia ya Fonolojia Boreshi. Irabu hizi zinatumika kuzalisha aina nyingi ya maneno ya *Sheng'*. Maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine yanakuwa umbaoghafi. Yakitokea katika *Sheng'* baada ya kuchukua irabu **/ɛ/** na **/ɔ/,** yanakuwa umbotokeo. Neno *mabao* likitamkwa katika hali ya kawaida humaanisha *idadi nyingi ya goli zilizofungwa katika mchezo wa kandanda*. Hata hivyo, neno hili likitamkwa na kubadilisha sauti **/o/** na kuwa **/ɔ/;** mauba**ɔ** litakuwa na maana ya *njaa*. Mifano ifuatayo yaweza kuthibitisha haya.

**Jedwali 20: Maneno yenye toni katika S.E.D**

| **Neno** | **Maana** |
|---|---|
| Bako | Kipimo cha kitanga cha mkono |
| Bak ɔ | Mpira wa vikapu |
| Bano | Chombo cha kubania mbao/chuma |
| Ban ɔ | Aina fulani ya jiwe |
| Bango | Karatasi kubwa ya maandishi |
| Bang ɔ | Shilingi moja |

Kutokana na jedwali hili, tumebainisha baadhi ya maneno ambayo yana silabi zinazokaribiana kimatamshi ila tu irabu **/ɔ/**. Irabu hii ndio inayochangia kuzuka kwa toni katika maneno haya. Wazungumzaji wa KS wasiokuwa na uwezo wa kutofautisha sauti hizi kimatamshi huenda wakaathirika kwa kushindwa kufahamu maana kusudiwa. Hali hii huweza kuchangia katika kuathirika kwa KS kifonolojia.

## HITIMISHO

Katika makala haya tumeainisha namna msimbo wa *Sheng'* unavyotofautiana kifonolojia na KS. Tumebainisha namna fonimu za *Sheng'* zinavyodhihirika katika irabu na konsonanti. Tumeonyesha aina mbalimbali za irabu za *Sheng'* na namna zinavyoshiriki kuunda aina tofauti za Silabi. Miundo ya fonimu za konsonanti za *Sheng'* zimeonyeshwa.

Tumeweza kuonyesha jinsi irabu na konsonanti za *Sheng'* zinavyotofautiana na za KS. Kadhalika, tumechunguza namna fonimu za *Sheng'* zinavyohusika katika uundaji wa silabi na viambishi mbalimbali vya maneno katika *Sheng'*. Tumeweza kuonyesha namna fonimu za *Sheng'* zinavyoshiriki katika uundaji wa aina mbalimbali za maneno ya *Sheng'*. Aina za maneno tulizobainisha ni nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi. Aidha, sura hii imefanikisha kuonyesha mifanyiko mbalimbali ya fonimu za *Sheng'*. Mifanyiko hii ni pamoja na: kuhafifika kwa fonimu, usilimishwaji wa fonimu, udondoshaji wa silabi na tangamano la irabu**.** Sifa za kiarudhi pia zimejadiliwa katika sura hii. Tumedhihirisha kuwa shadda katika *Sheng'* hujitokeza katika mazingira tofauti na namna ilivyo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.872

katika KS. Isitoshe, tumeonyesha namna kigezo cha toni kinavyosababisha tofauti za kifonolojia katika baadhi ya maneno ya *Sheng'* na KS. Tumehusisha uchunguzi wetu na mihimili ya nadharia ya Fonolojia Boreshi. Tumeonyesha jinsi maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine yanavyotumika kama umboghafi. Katika *Sheng'*, maneno haya hupitia taratibu mbalimbali za kifonolojia. Taratibu hizi tumezionyesha kuwa baadhi ya mashartizuizi kwa mujibu wa nadharia ya Fonolojia Boreshi. Maneno ambayo yanazalika baada ya kupitia taratibu hizi yanakuwa umbotokeo baada ya kuamuliwa na mhimili wa uzalishi. Hali hii inaonyesha kuwa, nadharia ya Fonolojia Boreshi, imefaa zaidi katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Kwa kufanya hivyo, lengo la utafiti huu ambalo ni kuonyesha tofauti za kifonolojia kati ya *Sheng'* na KS limetimika. Tumeweza kueleza hatua kwa hatua namna miundo mbalimbali ya fonimu za KS na *Sheng'* inavyotofautiana. Tumeonyesha pia namna silabi za *Sheng'* na KS zinavyotofautiana. Kadhalika, tumeonyesha namna sifa za kiarudhi za *Sheng'* zinavyokuwa tofauti na KS.

**MAREJELEO**

Bosire, M. (2006). *Hybrid languages: The Case of Sheng* State University of New York, Albany.

Ferrari, A. (2014). *Evolution of Sheng during the Last Decade*. Les Cahiers d'Afrique de l'Est / The East African Review, 49 | 2014, 29-54.

Githiora, C. (2018). *Sheng': Rise of a Kenyan swahili vernacular*. London: James Currey.

Kindija, K. (2012). *Taaluma ya fonetiki na fonolojia*. Dar es Salaam. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Makini, N. (2015). Udhihirikaji wa kanuni ya DAHL katika lugha ya Ekegusii. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Mgullu, R. (1999). *Mtaala wa Isimu. Fonetiki, na fonolojia*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugambi, A. (2007). *Utohozi maana katika maneno ya Sheng'*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mwihaki, A. (2007). Viewing *Sheng'* as a Social Dialect: A Linguistic Approach. International Journal of the School of Humanities and Social Sciences. Chemchemi Kenyatta University Vol.4 namba2.

Owino, A. (2016). Mifanyiko ya kimofofonolojia ya ukuzaji na udunishaji nomino za Kiwanga, Kakamega, Kenya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Egerton. Haijachapishwa.

Prince, A. & Smolensky, P. (2003). *Optimality theory in phonology*. Oxford: Oxford University Press

**Maelezo ya Istilahi**

**KS** – Kiswahili sanifu;

**Lugha changizi** – Lugha ambayo hutoa maneno ili yakubalike katika lugha ya pili

**Lugha pokezi** – Lugha inayopokea maneno ya mkopo kutoka lugha changizi.

**Mashartizuizi** – Vizuizi vinavyofanya neno fulani likubalike au lisikubalike katika lugha pokezi.

**Umbotokeo** – Neno lenye umboghafi ambalo halijaboreshwa na kukubalika katika lugha pokezi.

**Umboghafi** – Neno ghafi ambalo halijapitia vizuizi vya lugha kabla ya kukubalika katika lugha sanifu.

**Sheng'** – Msimbo wa lugha ya Kiswahili ambao asili yake ni mchanganyiko wa maneno ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji na ambao chimbuko lake ni mitaa ya mabanda jijini Nairobi.

**S.E.D** - *Sheng'* - English Dictionary

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.